KAULI YA TAARIFA YA CHANJO

# Chanjo ya Meningococcal ACWY: *Unachohitaji Kujua*

Many Vaccine Information Statements are available in Swahili and other languages. See www.immunize.org/vis

Kauli nyingi za taarifa ya chanjo zinapatikana katika Kiswahili na lugha nyinginezo. Angalia www.immunize.org/vis

## 1. Kwanini unahitaji kuchanjwa?

**Chanjo ya Meningococcal ACWY** inaweza kusaidia kukinga dhidi ya **ugonjwa wa meningococcal** unaosababishwa na vikundi vya sero A, C, W, na Y. Aina tofauti ya chanjo ya meningococcal inapatikana ambayo inaweza kusaidia kukinga dhidi ya kundi la sero B.

**Ugonjwa wa meningococcal** unaweza kusababisha meningitis (maambukizo kwenye utandu wa ubongo na uti wa mgongo) na maambikizo kwenye damu. Hata wakati umetibiwa, ugonjwa wa meningococcal huua watu 10 hadi 15 walioambukizwa kati ya 100. Na kati ya wale wanaoponea, karibu 10 hadi 20 kati ya kila 100 watapata ulemavu kama vile kupoteza uwezo wa kusikia, kuharibika ubongo, kuharibika figo, kupoteza maungo, matatizo ya mfumo wa neva, au makovu mabaya sana kutokana na kupachikwa ngozi.

Ugonjwa wa meningococcal ni nadra na umepungua Marekani tangu miaka ya 1990s. Walakini, ni ugonjwa mbaya sana wenye hatari kubwa ya kifo au ulemavu wa kudumu katika watu wanaoupata.

Mtu yeyote anaweza kupatwa na ugonjwa wa meningococcal. Baadhi ya watu huwa katika hatari zaidi, ikijumuisha:

- Watoto wachanga chini ya umri wa mwaka mmoja
- Vijana na watu wazima wachanga wa umri wa miaka 16 hadi 23
- Watu walio na magonjwa fulani yanayoathiri mfumo wa kinga
- Wanamikrobiolojia ambao hufanya kazi na isolates za *N. meningitidis*, bakteria ambayo husababisha ugonjwa wa meningococcal
- Watu walio katika hatari kutokana na kuzuka kwa ugonjwa katika jamii yao

## 2. Chanjo ya Meningococcal ACWY

**Vijana** wanahitaji dozi 2 za chanjo ya Meningococcal ACWY:

- Dozi ya kwanza: umri wa miaka 11 au 12
- Dozi ya (nyongeza) pili: umri wa miaka 16

Kwa kuongezea chanjo ya kawaida ya vijana, chanjo ya Meningococcal ACWY inapendekezwa kwa **vikundi fulani vya watu**:

- Watu walio katika hatari kwa sababu ya kuzuka kwa ugonjwa wa meningococcal ya serogroup A, C, W, au Y
- Watu walio na HIV
- Mtu yeyote ambaye wengu lake limeharibika au limeondolewa, ikijumuisha watu walio na ugonjwa wa selimundu
- Mtu yeyote aliye na hali nadra ya mfumo wa kinga iitwayo "complement component deficiency"
- Mtu yeyote anayetumia aina ya dawa inayoitwa "complement inhibitor," kama vile eculizumab (pia inayoitwa "Soliris"®) au ravulizumab (pia inayoitwa "Ultomiris"®)
- Wanamikrobiolojia ambao hufanya kazi na isolates za *N. meningitidis*
- Mtu yeyote anayesafiri kuenda au anayeishi katika sehemu ya ulimwengu ambayo ugonjwa wa meningococcal ni wa kawaida, kama vile sehemu za Afrika
- Wanachuo wapya wanaoishi katika kumbi za makazi ambao hawajachanjwa kikamilifu kwa chanjo ya Meningococcal ACWY
- Makurutu wa jeshi la Marekani

U.S. Department of Health and Human Services
Centers for Disease Control and Prevention

## 3. Zungumza na mtoa huduma za afya wako

Mwambie mtoa huduma ya chanjo wako ikiwa mtu anayepokea chanjo:

- Amekuwa na **mmenyuko wa mzio baada ya dozi ya awali ya chanjo ya Meningococcal ACWY**, au ako na **mmenyuko wowote mbaya sana wa mzio, wa kutishia maisha**

Katika baadhi ya visa, mtoa huduma za afya wako anaweza kuamua kuahirisha chanjo ya Meningococcal ACWY hadi katika ziara ya baadaye.

Kuna taarifa finyu kuhusu hatari za chanjo hii kwa wajawazito au watu wanaonyonyesha, lakini hakuna wasiwasi wa kiusalama umegunduliwa. Mtu mjamzito au ananyonyesha anapaswa kuchanjwa ikiwa imependekezwa.

Watu walio na magonjwa madogo madogo, kama vile mafua, wanaweza kuchanjwa. Watu ambao ni wagonjwa kwa wastani au wagonjwa vibaya wanapaswa kwa kawaida kungojea hadi wapone kabla ya kupokea chanjo ya meningococcal ACWY.

Mtoa huduma za afya wako anaweza kukupatia habari zaidi.

## 4. Hatari za mzio dhidi ya chanjo

- Wekundu au maumivu kwenye eneo la sindano vyaweza kutokea baada ya chanjo ya Meningococcal ACWY.
- Asilimia ndogo ya watu wanaopokea chanjo ya Meningococcal ACWY hupatwa na maumivu ya misuli, maumivu ya kichwa, au uchovu.

Watu huzirai wakati mwingine baada ya taratibu ya kimatibabu, ikijumuisha uchanjwaji. Mwambie mtoa huduma wako ikiwa unahisi kisunzi au mabadiliko katika kuona kwako au kuhisi milio masikioni.

Kama ilivyo na dawa yoyote ile, kuna uwezekano nadra sana kwa chanjo kusababisha mmenyuko mbaya wa mzio, majeraha mengine mabaya, au kifo.

## 5. Na je, kukiwa na tatizo hatari?

Mmenyuko wa mzio unaweza kutokea baada ya mtu aliyechanjwa kuondoka kliniki. Ikiwa utaona ishara za mmenyuko mbaya wa mzio (mabaka, kuvimba uso na koo, matatizo ya kupumua, moyo kudunda kwa kasi, kizunguzungu, au udhaifu), pigia simu **9-1-1** ili mtu huyo apelekwe kwenye hospitali iliyo karibu.

Kuhusu ishara zingine ambazo zinakupatia wasiwasi, pigia simu mtoa huduma za afya wako.

Mizio hatari inapaswa kuripotiwa kwa Mfumo wa Kuripoti Matukio Mabaya ya Chanjo (Vaccine Adverse Event Reporting System - VAERS). Mtoa huduma za afya wako kwa kawaida ataweka faili ya ripoti hii, au unaweza kufanya hivyo mwenyewe. Tembelea tovuti ya VAERS katika **www.vaers.hhs.gov** au piga simu **1-800-822-7967**. *VAERS ni ya kuripoti mizio pekee, na wafanyikazi wa VAERS hawapeani ushauri wa kimatibabu.*

## 6. Mpango wa Kitaifa wa Ufidiaji wa Majeraha ya Chanjo

Mpango wa Kitaifa wa Ufidiaji wa Majeraha ya Chanjo (National Vaccine Injury Compensation Program - VICP) ni mpango wa serikali kuu ambao ulibuniwa ili kufidia watu ambao huenda walijeruhiwa na baadhi ya chanjo. Madai kuhusiana na majeraha au vifo vinavyodaiwa kutokana na kuchanjwa yako na kikomo cha muda kwa kufaili, ambao unaweza kuwa mchache kama vile miaka miwili. Tembelea tovuti ya VICP katika **www.hrsa.gov/vaccinecompensation** au piga simu **1-800-338-2382** ili kujifunza kuhusu mpango huu na kufaili dai.

## 7. Je, ninawezaje kujifunza mengi zaidi?

- Muulize mtoa huduma za afya wako.
- Pigia simu idara ya afya eneo lako au ya jimbo.
- Tembelea tovuti ya Utoaji wa Chakula na Dawa (Food and Drug Administration - FDA) upate machapisho ya vifurishi vya chanjo na taarifa ya ziada katika **www.fda.gov/vaccines-blood-biologics/vaccines**.
- Wasiliana na Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa (Centers for Disease Control and Prevention - CDC):
  - Pigia simu **1-800-232-4636** (**1-800-CDC-INFO**) au
  - Tembelea tovuti ya CDC katika **www.cdc.gov/vaccines**.

Swahili translation provided by Immunize.org